TANGAZO LA SERIKALI Na. 142 la tarehe 28/2/2025

SHERIA YA MAMLAKA NA MAJUKUMU YA MSAJILI WA HAZINA,
(SURA YA 370)

# HATI YA UHAMISHO

(*Imetengenezwa chini ya kifungu cha 7(2))*

UHAMISHO WA UMILIKI WA NYUMBA ILIYOPO KATIKA KIWANJA NAMBA 403 MSASANI PENISULA CHENYE HATI NAMBA 17688 KUTOKA SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA (NHC) KWENDA WAKALA WA MAJENGO TANZANIA (TBA)

Sura ya 370 na. Sura ya 257

AMBAPO, kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina ikisomwa pamoja na Sheria ya Mashirika ya Umma, mali zote za Serikali zimewekwa Chini ya Umiliki wa Msajili wa Hazina;

NA AMBAPO, Serikali imeona kuwa inafaa kwamba Nyumba iliyopo katika Kiwanja Namba 403 chenye Hati Milki Namba 17688 kilichopo Msasani Penisula katika Halmashauri ya Manispaa ya Kinodnoni Jijini Dar es salaam ambacho kipo chini ya Umiliki wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kuhamishiwa kwa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA);

HIVYO BASI, imeelekezwa kama ifuatavyo:

Jina

1. Hati hii itajulikana kama Hati ya Uhamisho wa Nyumba iliyopo katika Kiwanja Namba 403 chenye Hati Milki namba 17688 kilichopo Msasani Penisula katika Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni Jijini Dar es salaam ambacho kipo chini ya umiliki wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kwenda kwa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ya mwaka 2025.

Uhamisho wa Nyumba

2. Nyumba iliyopo katika Kiwanja Namba 403 chenye Hati Milki Namba 17688 kilichopo Msasani Penisula katika Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni

Jijini Dar es salaam ambacho kipo chini ya umiliki wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), bila uthibitisho wa ziada na kuanzia tarehe ya kuanza kutumika kwa Hati hii, inahamishiwa kwa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA).

JEDWALI

(*Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| Mkoa | Hati Na. | Hati Milki na Maelezo ya Kiwanja | Taasisi inayohamishiwa |
|---|---|---|---|
| Dar es salaam | 17688 | Kiwanja Na. 403, Msasani Penisula, Wilaya Kinondoni | Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) |

**KWA AMRI YA RAIS**

Dodoma,
31 Januari, 2025

MOSES M. KUSILUKA,
*Katibu Mkuu Kiongozi*